

Dkt Mpango aweka jiwe la msingi ujenzi Kituo Mahiri cha Mazao ya Nafaka Kongwa

Na Bernadetha Mwakilabi, Kongwa

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kwa dhati kuboresha na kuinua uzalishaji katika kilimo na kwa sehemu kubwa itapunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa.

Dkt Mpango ameeleza hayo alipokuwa akiweka jiwe la msingi ujenzi wa kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka kilichopo kata ya Mtanana wilayani Kongwa mkoani Dodoma ambapo amefafanua kuwa Watanzania wamepata mwarobaini wa afya zao kwani mradi huo utatumika kudhibiti Sumukuvu.

Licha ya pongezi kwa Wizara ya Kilimo juu ya ujenzi wa kituo hicho Dkt Mpango ameagiza wizara kujenga bwawa kubwa kwaajili ya kudhibiti maji mengi yanayopotea kipindi cha Masika katika eneo la Mtanana lililoko wilayani Kongwa ili kuondoa adha ya mafuriko ya mara kwa mara na kukuza kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima.

Dkt Mpango ameelekeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Bodi za Nyama na Maziwa kuhakikisha mazingira ya soko la mifugo yanakuwa ya haki na uhalisia kwa kuhakikisha vipimo halali vinatumika katika minada ya mifugo ili kuondoa unyonyaji kwa wafugaji.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (kulia) akizindua ujenzi wa kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka

kilichopo Kata ya Mtanana wilayani Kongwa. (Picha na Bernadetha Mwakilabi).

Kwa upande wake Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe alisema kuwa hakuna Tanzania yenye sumukuvu tena kwa uwepo wa kituo hicho na kwamba atahakikisha anadhibiti mbegu feki kwa upatikanaji wa mbegu bora, mfumuko wa bei za mbegu kwa kufuata bei elekezi ili kuwaleta tija kwa kulima kwa kuzalisha mazao mengi.

Aidha Bashe aliongeza kuwa ndani ya kituo hicho kutakuwepo kiwanda cha kuchakata unga ambacho kitaruhusu wakulima wadogo kuchakata mahindi kwa gharama nafuu zaidi na kuwauzia wateja wao, kuwepo kwa vifaa vya kilimo ambapo wakulima wataodi kwa bei nafuu na pia zitatengwa ekari 45 kwaajili ya kufundisha wakulima jinsi ya kuzuia sumukuvu kwenye mazao kuanzia shambani.



Kutoka kushoto ni Naibu Waziri wa Kilimo Mh David Silinde, Waziri wa Kilimo Mh Hussein Bashe, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh Dkt Philip Mpango, Msimamizi wa Mradi kutoka TANIPAC ndugu Clipin Josephat, mkuu wa mkoa wa Dodoma Mh Rosemary Senyamule, Mnek Dodoma Donald Mejitii na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kongwa Mh White Zuberi. Picha na Bernadetha Mwakilabi.

Akiongea kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kongwa spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mbunge wa Jimbo la Kongwa Mheshimiwa Job Ndugai alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan na wote waliofanikisha mradi huo na kusema kuwa wanakongwa wanauthamini sana.

Vilevile aliongeza kuwa awali watu wengi walipoteza maisha kwasababu ya ugonjwa wa kansa ya ini unaosababishwa na ulaji wa vya kula vyenye sumukuvu lakini mradi huu umekuja kuwa

na suluhisho la magonjwa hayo.

Nae mfadhili wa mradi huo kutoka benki ya maendeleo Afrika (ADB) Mhandisi Alhaji Abdul Azpe Bangura alisema kuwa mradi huo utasaidia usalama na upatikanaji wa chakula, kubadili kilimo kuwa biashara kwa kuwatoa wakulima wadogo katika umasikini na kufanya serikali ya Tanzania kufikia malengo yake ya dira ya Taifa ya maendeleo kufikia 2050.

Mradi wa kituo hicho cha Umahiri wa Usimamizi wa Mazao ya Nafaka uliogharimu fedha TSh Bil 18 utasaidia wakulima zaidi ya 12,517 waliopata elimu ya kuzuia sumukuvu katika mkoa wa Dodoma na kusaidia kuboresha na kuinua uzalishaji wa kilimo kwa Taifa kwa ujumla.



Picha ikionesha eneo la kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka - Mtanana, Kongwa.







